MAELEZO SAHIHI

MUONGOZO WA REDIO

MUONGOZO WA SHUGHULI ZA KIJAMII

MAGONJWA YA KITROPIKI YALIYOSAHAULIKA

Tanzania

CHILDREN'S RADIO FOUNDATION

UTANGULIZI

Magonjwa ya kitropiki yaliyosahaulika (Neglected Tropical Diseases au NTDs) ni magonjwa yanayosababishwa na bakteria na vimilea ambukizi ambavyo hupatikana katika nchi 149 (https://bit.ly/3bVxWsd) ambazo huhesabika kutokana na hali yao ya anga kama nchi za kitropiki (zenye joto) kabisa au wastani. Magonjwa haya yanaleta athari hatarishi usumbufu mkubwa, na husababisha matatizo kama upofu au matatizo ya tumbo. Magonjwa yaliyosahaulika ya kitropiki huleta vifo zaidi ya 170,000 kwa mwaka, na watu zaidi ya bilioni huhitaji matibabu ya magonjwa haya (https://bit.ly/33tylhE).

Kinachosababisha kuenea kwa magonjwa ya kitropiki yaliyosahaulika (Neglected Tropical Diseases):
Magonjwa ya kitropiki mara nyingi husababishwa na ukosefu wa usafi wa mazingira na upatikanaji wa maji safi, makaazi, na chakula. Hali hii inasababishwa na ukosefu wa maendeleo na umasikini uliosababishwa na msingi wa ukoloni. Nchi nyingi zinazoathiriwa na magonjwa ya kitropiki barani Afrika zina historia za ukoloni, unyonyaji na uporaji wa rasilimali nyingi zilizojenga nchi na maendeleo ya ulaya. Hii imeleta athari za muda mrefu zinazotatiza njia ambazo serikali za Kiafrika zinaweza kujenga miundombinu ya afya kwa umma na usafi tangu zipate uhuru.

Kuna magonjwa matano makuu ya kitropiki yaliyoshaulika ambayo yanaathiri ulimwengu sana. Magonjwa hayo ni:

1. Minyoo tumboni (intestinal worms)
Huu ndio ugonjwa wa kitropiki uliosahaulika unaojulikana zaidi kuliko mengine ulimwenguni kote, na zaidi ya waathirika bilioni 1.7 wanahitaji matibabu. Minyoo ya tumboni mara nyingi huenezwa kupitia kwa vyakula au vinywaji vichafu. Minyoo huishi na kuhamishwa kupitia udongo na kinyesi cha binadamu, kwa hivyo wakati maji safi hayapatikani, kuna hatari kubwa ya maambukizo na ueneaji. Minyoo husababisha uharibifu kwa kutaga mayai ndani ya miili yetu, ambayo inaweza kusababisha maumivu mwilini au kutokwa damu kwenye njia za kupitisha chakula tumboni. Kutokwa na damu tumboni basi husababisha upungufu wa damu (anaemia), utapiamlo, uvimbe wa tumbo, upotezaji uzito wa kimwili, kuhara, na mengine mengi (https://bit.ly/3bW9g2C).

2. Ugonjwa wa kichocho (Schistosomiasis)
Ugonjwa wa kichocho (Schistosomiasis) au Bilharzia ni ugonjwa wa kitropiki wa pili unaojulikana zaidi, na unaambukizwa kwa kugusana na maji ambayo yameambukizwa na vimelea ambavyo huishi kwenye konokono ambao huishi katika maji, kwa mfano mito na mifereji; vimelea hivi hupenya katika ngozi na kuingia mwilini. Ingawa ni ugonjwa wa kitropiki uliosahaulika na wa pili unaojulikana zaidi, ndio ugonjwa unayosababisha vifo vingi zaidi na zaidi ya waathirika milioni 228 ulimwenguni kote wanahitaji matibabu (https://bit.ly/2RorBfr).

3. Ugonjwa wa Matende (Lymphatic Filariasis)
Ugonjwa wa Matende (Lymphatic filariasis) ni ugonjwa wa kitropiki ambao unaweza ukawa hauna dalili zinazoonekana, daili kidogo tu, na dalili sugu katika mwili. Ugonjwa huu wa matende mara nyingi huitwa ‘elephantiasis’ na hutambulika sana kutokana na athari zake kwenye mwili.

Ugonjwa wa Matende unaweza kusababisha uvimbe mkali katika viungo vya mwili, kama mikono na miguu, ambao husababisha usumbufu mkali na ulemavu (https://bit.ly/3ixhAIE). Maambukizi ya ugonjwa huu huenezwa na mbu na vimelea, na unaweza kuambukizwa wakati wa utotoni na kisha kujitokeza baadaye kabisa ukiwa mtu mzima (https://bit.ly/3itxTGH).

4. Trakoma inayopofusha (Blinding Trachoma)

Trakoma inayopofusha ni maambukizi ya macho ya kibakteria ambayo husababisha upofu. Ndio sababu kuu inayoongoza ya kusababisha upofu wa kuambukizwa ulimwenguni kote, na pia ni sababu ya pili kuu ya upofu kiujumla (https://bit.ly/33txoWC). Ugonjwa huu unaenea kupitia kugusana moja kwa moja na watu ambao wameambukizwa, na pia kuwasiliana na nzi. Ikiwa haijatibiwa, ngozi inayoshikilia kope machoni hugeuka ndani na kisha kope kukwaruza katikati ya jicho (sehemu ya 'cornea') na kusababisha maumivu makali na usumbufu mwingi, na mwishowe upofu. Zaidi ya watu milioni 142 walioathirika wanahitaji matibabu.

5. Ugonjwa wa upofu wa macho unaosababishwa na wadudu wa kwenye mto (River Blindness)

Ugonjwa wa upofu wa macho usababishwao na wadudu kwa kwenye mto, ujulikanao pia kama 'Onchocerciasis,' ni maambukizi ya macho na ngozi ambayo husababishwa na vimelea vinavyosambazwa na kuumwa na nzi mweusi (https://bit.ly/3kgKCgd). Nzi mweusi huishi na kuzaliana kwenye mito mikubwa na midogo midogo, na hapo ndipo pia ugonjwa huu hupatikana na umepatiwa jina hilo (https://bit.ly/32tDYxi). Ingawa ugonjwa huu unasababisha upofu kwa kiwango kidogo kuliko trakoma, kuna zaidi ya watu milioni 217 wanaohitaji matibabu ya ugonjwa huu duniani.

ONDOA UZUSHI!

UZUSHI	UKWELI
Ni watu wazima ambao ndio hasa wanaugua na kuathiriwa na magonjwa ya kitropiki yaliosahaulika kwa kiasi kikubwa	Watoto bilioni1 ulimwenguni wanaugua magonjwa ya kitropiki yaliosahaulika.
Magonjwa ya kitropiki yaliosahaulika ni shida ya kiafya tu	Pindi jamii zinapokuwa na viwango vya juu vya maambukizi na / au ulemavu unaotokana na magonjwa ya kitropiki yaliyosahaulika, watu na jamii kwa ujumla hutumia fedha nyingi, nguvu na akili ili kuyakabili maradhi haya. Matibabu ya magonjwa ya kitropiki yaliyosahaulika ikiwa hayapatikani katika eneo hilo inaweza kusababisha gharama kubwa, pamoja na usafiri ili kufikia sehemu yenye huduma hiyo, na kuletea familia shida za kifedha. Watu wazima wanaofanya kazi ambao wanapata magonjwa ya kitropiki yaliyosahaulika hawawezi tena kufanya kazi zao, na hii inaweza kuathiri mapato ya familia zao kwa ukosaji wa ada ya shule, kodi, vyakula na kadhalika. Watoto ambao wanakabiliwa na maumivu sugu ya magonjwa ya kitropiki yaliyosahaulika pia wanaweza kushindwa kuhudhuria masomo yao shuleni kwa muda wa wiki hadi miezi, na kuwa na wakati mgumu sana wa kumaliza masomo kulingana na ratiba ya masomo, na vile vile hupata ugumu kupata marafiki na kushiriki katika jamii zao.
Magonjwa ya kitropiki yaliyosahaulika hayaathiri maendeleo ya nchi au jamii	Magonjwa ya kitropiki yaliyosahaulika yanaweza kubebesha jamii mzigo na gharama kubwa za kiafya, maumivu sugu na kutokuwa na uwezo wa kufanya kazi. Katika jamii ambazo umasikini umeenea na upatikanaji wa huduma bora za afya ni mdogo, utunzaji wa wagonjwa unaweza kuwa mgumu na kupunguza fursa za watu kuepuka umaskini kupitia kazi na elimu, au kwa maneno mengine, kupaa/kufanikiwa kimaisha.
Magonjwa yote ya kitropiki yaliyosahaulika yanaua	Sio magonjwa yote ya kitropiki yaliyosahaulika ambayo husababisha kifo. Ingawa magonjwa haya mengi yanaweza kusababisha ulemavu mkali/ wa kudumu, mengine yanaweza kuwa na athari nyepesi au hata dalili tu. Kinga ni njia bora ya kutokomeza magonjwa ya kitropiki yaliyopuuzwa, lakini matibabu yanaweza kusaidia sana kudhibiti dalili na maumivu yanayosababishwa na magonjwa haya.

IKO VIPI KUISHI NA UGONJWA WA KITROPIKI ULIOSAHAULIKA

Haimamote Debebe ni mwanamke kutoka Ethiopia ambaye anaishi katika eneo la mashambani liitwalo Mekelle. Kama mtu mzima, Haimamote angeendelea na utaratibu wake wa kila siku wa kusafisha na kutunza mifugo, hadi alipoanza kupata maumivu ya kichwa na macho. Kwa muda mrefu, maumivu haya yalikuwa dalili ya trakoma na kuona kwake kukaanza kuzorota. Kuishi na maumivu sugu na ulemavu kama upofu kumebadilisha maisha ya Haimamote sana na uwezo wake wa kujishirikisha katika maisha vile angependa, sembuse kuwa sasa hata hawezi tena kufanya kazi na kuchangia utunzaji wa familia yake (https://bit.ly/3kjOgpN).

MWITIKIO WA KATIKA MATIBABU NA KINGA YA MAGONJWA YA KITROPIKI YALIYOSAHAULIKA

Katika nchi kama Ethiopia (https://bit.ly/2GS8ecA) na Zambia (https://bit.ly/3mlMJRG) watu tofauti wamekusanyika pamoja kutafuta suluhisho kwa jamii zao. Banchayehu Kassie ni mfanyakazi wa afya katika eneo la Lay Gayint nchini Ethiopia, ambapo hutumikia jamii ya watu 1,500. Kazi yake ni kutoa na kusimamia dawa kwa familia, kuhimiza usafi wa mazingira na kibinafsi wakati inapowezekana, kama vile unawaji mikono na uso mara kwa mara, na kutoa mafunzo kwa wanajamii kuhusu udumishaji wa afya ili kupambana vizuri na kutibu magonjwa ya kitropiki yaliyosahaulika. Nchini Zambia, mfanyakazi wa taasisi ya kutoa huduma za msaada anayeitwa Robert Ntitima, pamoja na dereva wake, husafirisha madaktari wanaozunguka vijijini. Hii inawezesha madaktari kuweza kutembelea jamii zilizo mbali au zilizotengwa, na kuwafikishia huduma kama upasuaji kwa wagonjwa wa trakoma. Katika nchi hizi mbili, watu hufanya kazi pamoja ili kuleta suluhu kwa jamii ambazo zinazihitaji.

JE, WAJUA?

TANZANIA

- Wakati Watanzania milioni 16 tayari wanapokea matibabu ya magonjwa ya kichocho, trakoma, matende, na upofu unasababishwa na wadudu wa kwenye mito, bado watu milioni 9 kiujumla wanahitaji dawa na matibabu (https://bit.ly/3mlMJRG)

- Vijana nchini Tanzania wanaongoza juhudi za kumaliza magonjwa ya kitropiki yaliyopuuzwa. Mwaka 2020, zaidi ya vijana 150 walikusanyika Dar es Salaam, Tanzania kujadili jinsi ya kupambana na magonjwa ya kitropiki yaliyosahaulika katika kipindi cha maisha yao, na wakaunda kikundi cha kupambana na kutokomeza magonjwa haya kwa kizazi hiki kiitwacho: End Neglect and Commit to an NTD-Free Generation

JE, WAJUA?

ETHIOPIA

Mnamo mwaka 2015, kampeni ya kwanza ya kupambana na minyoo ilizinduliwa nchini Ethiopia, ambayo inakusudia kutibu watu milioni 20 wanaougua ugonjwa wa kichocho na minyoo mwishoni mwa mwaka huu. Njia moja ya kimkakati zaidi ya kupambana na kuenea kwa magonjwa ya kitropiki yaliyosahaulika shuleni ni kampeni za kuzuia minyoo, ambazo huwapatia watoto huduma za matibabu katika shule zao. (https://bit.ly/3mjYxUF)



ZAMBIA

- Zambia imeathirika hasa na magonjwa matatu ya kitropiki yaliyopuuzwa, kati ya matano yanayotambulika zaidi ulimwenguni kote. Magonjwa hayo matatu ni kichocho, trakoma, na matende. (https://bit.ly/3ioMqDn)
- Nchini Zambia, zaidi ya watu milioni 2.5 wanahitaji matibabu ya trakoma inayopofusha, na watoto milioni 4.5 wa shule wanahitaji matibabu ya minyoo.
- Zambia kwa sasa inafanya kazi chini ya mpango wa kitaifa wa kutokomeza magonjwa ya kitropiki nchini humo ifikapo 2023.

CÔTE D'IVOIRE

- Cote d'Ivoire (Ivory Coast) ni nchi iliyopo magharibi mwa Afrika yenye idadi ya watu milioni 26.4. Magonjwa ya kitropiki yaliyosahaulika yameenea katika maeneo mengi humo nchini na watu wanaokadiriwa kuwa milioni 23 wako hatarini kuambukizwa ugonjwa mmoja au zaidi wa kitropiki. Hii inaathiri vibaya wenye kipato cha chini na pia jamii zilizotengwa/zilizosahaulika (https://bit.ly/3miBgm3).
- 1 kati ya watu 6 nchini Cote d'Ivoire (Ivory coast) ambao wana trakoma wanahitaji matibabu.
- 45% ya watu nchini humo wanahitaji matibabu ya minyoo.
- Mnamo mwaka 2016, Ivory Coast iliunda mpango wa kitaifa wa kutokomeza magonjwa ya kitropiki nchini humo. Ingawa magonjwa ya kitropiki bado hayajaisha, vita ya kuyamaliza kabisa bado inaendelea.

JE, WAJUA?

JAMHURI YA KIDEMOKRASIA YA KONGO

- Nchini Kongo, ni 50% tu ya watoto walio kwenye hatari ya kupata minyoo ambao wanaweza kupata matibabu wanayohitaji.

- Kukomesha kuenea kwa magonjwa ya kitropiki yaliyosahaulika na kuyasimiamia ipasavyo
- inaweza kuwa ngumu katika maeneo ya vijiji vya Kongo, ambapo 69% ya watu katika maeneo haya hawana maji safi ya kunywa.

Shirika la Afya Duniani (WHO) linakadiria kuwa watu wapatao milioni 1.9 ni vipofu au kuona kwao kumeharibiwa na trakoma, na watu milioni 2.5 wanahitaji upasuaji ili kuzuia upofu.

WANAWAKE NA WASICHANA WANAATHIRIWA ZAIDI NA MAGONJWA YA KITROPIKI YALIYOSAHAULIKA

- Kulingana na ripoti ya 2016 ya Kuungana ili Kupambana na Magonjwa ya Kitropiki yaliyosahaulika, theluthi-mbili ya ukusanyaji/uchotaji wa maji hufanywa na wanawake na wasichana. Hii inawaweka katika hatarii kubwa sana ya kupatwa na magonjwa ya kitropiki yapatikanayo kwenye maji. (https://bit.ly/3iwpnqd)
- Wanawake na wasichana mara nyingi huchukuliwa kama watunza mji, na hii inaweza kuwasababishia kukosa: elimu, ajira, maisha, na afya (https://bit.ly/3kk7DyH).
- Jinsia pia inachangia katika jukumu la upishi na usafishaji: wanawake ulimwenguni kote mara nyingi hupewa majukumu ya nyumbani, ambayo hayathaminiwi na huwatia hatarini zaidi katika kuambikizwa magonjwa ya kitropiki: Utumiaji mkubwa zaidi wa maji ya kupikia na kusafisha huwasababishia hatari kubwa zaidi ya kupata magonjwa ya kitropiki.

KINACHOWEZA KUFANYWA ILI KUTOKOMEZA UENEAJI WA MAGONJWA YA KITROPIKI YALIYOSAHAULIKA:

1. Kupunguza unyanyapaa:

- Kukomesha unyanyapaa - ambao ni kuwa na ushirikiano hasi na aibu, ni jukumu la kila upande kusaidia wale ambao wameathiriwa na magonjwa ya kitropiki, na vile vile wale ambao walio nje ya nchi ambazo zinapambana na magonjwa haya. (https://bit.ly/32s1w5k)
- Sawa na unyanyapaa uliopo katika VVU, unyanyapaa katika kuambukizwa na kuishi na magonjwa ya kitropiki hufanya hali iwe ngumu kwa jamii kuelewa na kukabiliana na magonjwa haya ipasavyo. Ikiwa watu wanahofia aibu ya kuwa na magonjwa ya kitropiki, wanaweza kukaa kimya kuhusu kupata matibabu, na mwishowe kuweka afya zao na za wengine pia hatarini.
- Kukomesha unyanyapaa uliopo kwa sababu ya magonjwa ya kitropiki, na kuwa na elimu zaidi kuhusu jinsi yanavyoathiri watu pia, hupunguza unyanyapaa kuhusu umasikini barani Afrika. Badala ya kuona magonjwa ya kitropiki kama suala linaloathiri tu maeneo maskini barani, tunaweza kuuliza ni nini ambacho kimesababisha ukosefu wa maji safi katika nchi zingine katika bara letu na, ni nini ambacho tunapaswa kufanya ili kusuluhisha hilo. Ukosefu wa usafi wa mazingira na huduma za afya ni suala la haki za kibinadamu ambalo linastahili umakini, kusaidiana, na kutafuta ufumbuzi wa kijamii. Kusaidia taasisi na miradi ya msaada kupitia michango katika vyombo vya habari vya kijamii inaweza kusaidia kupambana na unyanyapaa wa magonjwa ya kitropiki, hasa katika nchi ambazo zina hatari kubwa.

2. Masuala ya maji na usafi wa mazingira na kibinafsi:

- Uwekezaji katika masuala ya maji na usafi wa mazingira na hasa unaweza kupatikana kupitia uwekezaji wa serikali za mitaa na pia misaada ya nje, hayo yote kwa msaada wa jamii za wenyeji. Kujenga miundombinu ya jamii safi kutakuwa na manufaa ya kudumu katika kupunguza kuenea kwa magonjwa ya kitropiki, na kwa kuenea kwa maumivu ya kimwili na mfadhaiko wa jamii usababishwao na magonjwa haya. (https://bit.ly/2GYqC3I)

TAFSIRI (UFAFANUZI)

- **Kukosa dalili (asymptomatic)** kunamaanisha kwamba wakati mtu ana maambukizi ya bakteria au virusi vya ugonjwa fulani, haonyeshi dalili zozote za kuwa ana ugonjwa, na hahisi makali yeyote pia. Ugonjwa wa matende ni mojawapo ya magonjwa haya ya kitropiki yaliyosahaulika ambayo watu wanaweza kuwa wanayo, lakini hawaonyeshi dalili.

- **Ueneaji (- borne)** inamaanisha jinsi ugonjwa fulani huambukizwa au kuenea. Kwa mfano, mojawapo ya magonjwa matano ya kitropiki yanayojulikana zaidi, Kichocho, huitwa 'vector-borne,' kumaanisha kwamba unasababishwa na vimelea, virusi na bakteria ambao hupitishwa na viumbe vinavyoitwa 'vectors.' Vectors ni viumbe-hai ambavyo vinaweza kupitisha/kubeba vimelea ambukizi kati ya binadamu mmoja hadi mwingine, au kutoka kwenye wanyama kwenda hadi kwa binadamu (https://bit.ly/3hvfDuY).

- **Ukoloni** ni 'mfumo wa nguvu' na pia zoezi la wazungu kudai nafasi ya mamlaka na kuwa na ubaguzi dhidi ya watu weusi. Ukoloni kwa ujumla unamaanisha vitendo vya dhuruma, kutawala watu, na utumwa wa kulazimishwa na wazungu katika nchi tofauti ulimwenguni. Ukoloni ulifanya mataifa huru barani Afrika kuwa kama 'mali' ya nchi za Ulaya, na kuwalazimisha watu weusi kufanya kazi ambazo ililetea nchi za Ulaya mapato na kuzalisha rasilimali ambazo zilitumiwa na viongozi wa kikoloni au kurudishwa kwa "nchi mama." Ukoloni uliacha athari kubwa za kifedha na rasilimali, pia kiakili. Vile vile, kwa watu weusi ambao walilazimishwa kuingia katika hali ya ukoloni. Pia, ukoloni uliunda hadithi ya kibaguzi na kuelekeza unyonge na dharau kwenye bara la Afrika. (https://bit.ly/3kf2sjF)

- **Kuambukizwa /maambukizi** ni neno lingine lenye maana ya kupata ugonjwa. Kwa mfano, unapoambukizwa ugonjwa wa kitropiki, inamaanisha kwamba umeupata kwa kuwasiliana na mtu mwingine, bakteria fulani au virusi.

- **Huduma za usafi** , sawa na usafi wa mazingira, ni aina ya vitu vinavyowafanya watu waweze kuendelea kuwa wasafi. Usafi unaweza kumaanisha upatikanaji wa sehemu za kunawa mikono, au bomba la maji safi na sabuni ili kuondoa viini kutoka katika mikono ya watu, macho, na midomo/vinywa vyao.

- **Miundombinu** inahusu ujumla wa mfumo au msingi wa taasisi fulani. Wakati kuna ukosefu wa rasilimali, kama vile fedha, malighafi, chakula na kilimo, nk, kuna ukosefu wa msingi wa kuweza kusaidia utendaji/ uendeshaji wa maisha ya kila siku kwa watu. Katika nchi ambazo magonjwa ya kitropiki yameenea, wakati mwingine kuna ukosefu fulani wa miundombinu ambayo imesababisha ukosefu wa usafi wa mazingira au kutoweza kutoa huduma ya afya. Miundombinu ya nchi maskini za Kiafrika sio ya ukweli wala kiasili au jambo la kawaida,

lakini ni matokeo ya mamia ya miaka ya unyonyaji rasilimali na ubaguzi wa rangi uliotokana na ukoloni.

- **Minyoo ya tumboni** ni minyoo ambayo huishi na huhamishwa kupitia udongo na kinyesi. Ikiwa mtu ataambukizwa minyoo kwa kuwasiliana na maji machafu ambayo yameambukizwa na minyoo, mara tu ikiingia mwilini, inaweza kutaga mayai ambayo yanaweza kusababisha madhara mwilini, na wakati mwingine hata shida zanazotishia maisha kutokana na uharibifu inayoosababisha (https://www.who.int/intestinal_worms/more/en/).

- **Vimelea (Parasite)** ni viumbe ambavyo huishi kwa kuchukua (kutegemea) kutoka kwa viumbe-hai vingine. Magonjwa ya kitropiki ni magonjwa ya vimelea, kumaanisha kwamba yapo, na yanaathiri wanadamu kwa kuchukua rasilimali kutoka mwilini, na hiyo ndio sababu huyafanya magonjwa ya kitropiki kuwa yenye uchungu/maumivu au makali zaidi kwa wale walio nayo. (https://www.medicinenet.com/script/main/art.asp?articlekey=4769**)**

- **Magonjwa ya Kitropiki yaliyopuuzwa/yaliyosahaulika** ni magonjwa ambukizi ya bakteria na vimelea, na magonjwa haya yapo katika nchi 149 ambazo huchukuliwa kuwa za kitropiki au zenye joto katika hali zao za tabia nchi. Inachukuliwa kuwa magonjwa haya yamepuuzwa/sahauliwa kwa sababu ya kuenea kwao zaidi, na kuathiri watu bilioni 1.7 ambao wanadhaniwa kuwa wanaishi katika umasikini, ikilinganishwa na ukosefu wa matibabu yanayopatikana kwa sababu ya ukosefu wa tiba kwa muda mrefu (tangu zamani), pamoja na unyang'anyi wa kikoloni wa rasilimali za nchi za Afrika. (https://bit.ly/2DXu9xW)

- **Usafi wa mazingira** unahusu usimamizi wa taka kama vile kinyesi cha binadamu au wanyama (yaani vyoo ambavyo hubeba taka lakini havichafui udongo au vyanzo vya maji) au mifereji inayofaa katika jamii ya kuruhusu maji kutoka nje badala ya kushindikana papo hapo na kuleta magonjwa. Usafi wa mazingira pia ni usafi wa nafasi, miundombinu, na mahali. Usafi wa mazingira ni sehemu muhimu ya kuzuia kuenea kwa magonjwa ya kitropiki na pia mengine kama COVID-19. Upatikanaji wa maji safi na chakula ni haki ya binadamu, na inazuia bakteria hatari na vijidudu vingine kuchafua rasilimali za jamii. (https://bit.ly/3mjkD9Q)

- **Unyanyapaa** ni hisia hasi, maoni, mitazamo na imani/itikadi ambazo husababisha watu kukataa, kuepuka au kuogopa watu wanaowaona kuwa tofauti (https://bit.ly/35BcYOi)

- **Masuala ya maji na usafi wa mazingira na kibinafsi (yaani, WASH)** ni kifupi ambacho husimamia maji, usafi wa mazingira na wa kibinafsi, na ni moja wapo ya mikakati muhimu ya kupambana na kumaliza kuenea kwa magonjwa ya kitropiki. (https://bit.ly/2RoukFB)

MAGONJWA YA KITROPIKI YALIYOSAHAULIKA
MUONGOZO WA VIPINDI VYA REDIO

MAANDALIZI YA KIPINDI CHA REDIO

Jinsi ya kuzungumza kuhusu magonjwa ya kitropiki yaliyosahaulika barani Afrika, na kwanini ni muhimu kuyajua na pia kupambana nayo.

- Magonjwa ya kitropiki yaliyosahaulika (Neglected Tropical Diseases - NTDs) ni yapi?
- Ni changamoto zipi na ufumbuzi gani wa nchi yangu kwa magonjwa ya kitropiki yaliyosahaulika?
- Unyanyapaa una jukumu gani katika kuenea kwa magonjwa ya kitropiki yaliyosahaulika?
- Ni sababu gani zinazoongoza kwa uwepo wa magonjwa matano makuu ya kitropiki yaliyosahaulika, na jamii zinawezaje kuyazuia kuenea?

CHAGUA MADA MAHUSUSI

Ni sababu gani zinazoongoza kwa uwepo wa magonjwa matano makuu ya kitropiki yaliyosahaulika, na jamii zinawezaje kuyazuia kuenea?

Jinsi ya kuzungumza kuhusu mada:

- Ongea kuhusu jukumu la jinsia katika kuweka watu fulani katika hatari kubwa zaidi kuliko wengine wa kuambukizwa magonjwa ya kitropiki.
- Ongea kuhusu mikakati ya matibabu na kinga ya magonjwa ya kitropiki katika jamii yako.
- Ongea kuhusu changamoto ambazo jamii yako inaweza kuwa inakabiliwa nayo/nazo katika kujaribu kudumisha afya bora na kutekeleza mazoea mazuri ili kuzuia maamubizi ya magonjwa ya kitropiki.
- Ongea kuhusu jinsi jamii yako inaweza kuungana pamoja ili kusaidia kuelewa hatari na mikakati ya kutokomeza usambazaji wa magonjwa ya kitropiki katika eneo lako kwa kutoa vidokezo vya kuunga mkono.

MIUNDO YA VIPENGELE VYA KIPINDI CHA REDIO

SAUTI ZA UMMA (VOX POPS)

Lengo la sauti za umma:
Kupata maoni mengi kuhusu mada moja

Utazungumza na nani:
Mtu yeyote kutoka katika jamii

Swali:

- Je, wajua kuhusu magonjwa ya kitropiki yaliyosahaulika na jinsi yanavyo enea? Kwa nini unafikiri ni muhimu watu wote wapate maji safi na usafi wa mazingira?

MAONI YA SAUTI

Lengo la maoni ya sauti:
Kupata maoni ya watu kuhusu mada ambayo wanaijali.

Utazungumza na nani:
Mtu yeyote kutoka katika jamii

Swali:

- Magonjwa ya kitropiki yaliyosahaulika yanaathiri jamii nyingi maskini zenye ukosefu wa rasilimali; unafikiri jamii yako ina rasilimali nzuri za kimatibabu na kiafya? Je, wewe hufanyaje ili kutunza afya yako na ya wale walio karibu nawe?

WASIFU WA SAUTI

Lengo la wasifu wa Sauti:
Wasikilizaji wasikie hadithi ya kuhamasisha kuhusu mada ya kipindi.

Utazungumza na nani?
Kijana aliyeathrika na magonjwa ya kitropiki mwenyewe, au kupitia kwa jamii yake.

Maswali ya kuuliza ili kumfanya mtu atafakari kwanza, kabla ya kurekodi wasifu wake:

- Ni magonjwa yapi ya kitropiki ambayo yamekuathiri wewe au jamii yako?
- Kuna mahali ambapo unaweza kwenda ili kupata matibabu? Je, unadumishaje usafi wa mikono yako au maji yako?
- Ni nini kinaweza kuboreshwa ili kupambana na kuenea kwa magonjwa ya kitropiki?
- Kwa nini afya yako ni jambo la muhimu kwako?
- Jamii yako inachangia/inatoa ufumbuzi gani ambao unahakikisha kuwa kuna upatikanaji wa maji safi na usafi wa mazingira?

AU

- Utazungumza na nani: Mhudumu wa afya katika kliniki yako ya karibu anayejua kuhusu magonjwa ya kitropiki au mfanyakazi wa taasisi ya afya au mradi unaoshugulikia masulala ya magonjwa ya kitropiki.

- Maswali ya kuuliza ili kumfanya mtu atafakari kwanza, kabla ya kurekodi wasifu wake:
  - Historia yako ni nini, umekuwa ukifanya hii kazi kwa muda upi?
  - Kwa nini magonjwa ya kitropiki ni shida kubwa sana?
  - Vijana wanawezaje kuwa na mazungumzo kuhusu magonjwa ya kitropiki na pia kupata uzoefu wa kudumisha afya nzuri ili kuzuia kuenea kwa Magonjwa haya?
  - Ni ufumbuzi upi wa kijamii ambao kwa maoni yako unaonelea kuwa ni bora?

TANGAZO LA UMMA (PSA)

Lengo la tangazo la umma ni:
Kuweka mwamko wa jamii kuhusu jambo fulani.

MAANDALIZI YA KIPINDI CHAKO

Tumia miundo ya vipengele na utafiti wako kuandika muongozo wako. Hapa kuna mfano wa sehemu ya muongozo. Unaweza kuutumia kama muongozo unapotayarisha maandalizi ya shughuli ya kijamii.

[UFUNGUZI WA KIPINDI:]

Mtangazaji 1: Hamjambo na karibuni [TAJA JINA LA KIPINDI] hapa [TAJA JINA LA STESHENI]. Jina langu ni [TAJA JINA LAKO].

Mtangazaji 2: Na jina langu ni [TAJA JINA LAKO], na kipindi chetu cha leo kinahusu magonjwa ya kitropiki yaliyopuuzwa/yaliyosahaulika - au 'Neglected Tropical Diseases' - NTDs kwa kifupi. Tunazungumza kuyahusu kwa sababu magonjwa haya yanaweza kuua na kuathiri jamii kwa njia ngumu sana, haswa jamii zilizotengwa na zilizokosa rasilimali na upatikanaji wa maji safi na usafi wa mazingira.

Mtangazaji 1: Magonjwa ya kitropiki yaliyosahaulika yanaathiri sehemu tofauti za ulimwengu, lakini zinajikita zaidi katika maeneo yenye hali joto ya hewa. Magonjwa ya kitropiki yameathiri bara la Afrika zaidi, haswa katika maeneo ya vijijini ya nchi kama Ethiopia, Tanzania, Zambia, na Kongo. Magonjwa ya kitropiki yaliyosahaulika ni ya muhimu kujua kwa watu ambao wameathiriwa nayo na pia wale ambao bado hawajaathiriwa, kwa sababu magonjwa haya husababisha vifo zaidi ya 170,000 kwa mwaka. Kilicho muhimu kujua hapa ni kwamba hii idadi kubwa ya vifo inaweza kuzuilika, kwa sababu kuenea zaidi kunatokana na ukosefu wa maji safi na usafi wa mazingira, kama unawaji mikono na uso.

Mtangazaji 2: Ni mantiki kabisa! Umaskini na ukosefu wa upatikanaji wa haki za msingi za binadamu ni suala kubwa kwetu sisi, na kama vijana tunapaswa kujali. Tunapaswa pia kujua kwamba umasikini katika bara la Afrika pia unasababishwa na ukoloni na rasilimali zote ambazo zilichukuliwa kutoka nchi nyingi ili kujenga nchi za Ulaya na Amerika ya Kaskazini. Kwa hivyo magonjwa ya kitropiki yaliyopuuzwa/yaliyosahaulika ni shida kubwa, na ni sehemu ya historia ya vurugu na ukosefu.

Mtaganzaji 1: Wakati magonjwa ya kitropiki yanaathiri jamii, yanaweza kusababisha usumbufu mwingi wa mwili na athari za kudumu, kama maswala ya kumeng'enya kwa muda mrefu (au, long term digestion problems) na upofu. Hii sio kama homa, ambayo mara nyingi dalili zinaweza kuondoka, lakini wakati mwingine hukaa kwa muda mrefu na kuathiri uwezo wa watoto kwenda shule na kupata mafunzo, au uwezo wa watu wazima kufanya kazi, kuwatunza wengine, na kuendeleza juhudi zao za kimaisha ya kila siku. Inadumisha umasikini katika jamii. Vijana kama sisi tunaweza kupata njia za kuunga mkono harakati za kutokomeza magonjwa ya kitropiki na kuenea kwao kwa kutetea michakato zaidi, miundo ya usafi wa mazingira na ya maji safi.

Mtangazaji1: Kwa hivyo, hebu kwanza tusikie kutoka kwa mfanyakazi wa kliniki ambaye anajua kuhusu na anayefanyia kazi magojwa haya ya kitropiki.
[TAJA ANAYEHOJIWA]
[CHEZA MAHOJIANO]

Maswali yaliyopendekezwa kwa mahojiano yako na mtu anayejua ukweli wa mambo:

- Historia yako ni ipi, umekuwa ukifanya hii kazi kwa muda upi?
- Kwa nini magonjwa ya kitropiki ni shida kubwa sana?
- Vijana wanawezaje kuwa na mazungumzo kuhusu magonjwa ya kitropiki na pia kupata uzoefu wa kudumisha afya nzuri ili kuzuia kuenea kwa magonjwa haya?
- Ni ufumbuzi upi wa kijamii ambao kwa maoni yako unaona kuwa ni bora?

[KUFUNGA KIPINDI:]

Mtangazaji1: Leo, tumesikia kuhusu magonjwa ya kitropiki yaliyosahaulika ni nini, athari zake, na suluhisho/ufumbuzi bora wa kupambana na kuenea kwao.

Mtangazaji 2: Ndio, na ni ya kufurahisha kujua kwamba kuna watu na watoa huduma za afya ambao wanafanya kazi ili kuelimisha na kutenda kazi katika jamii zao. Sasa ninaelewa dhahiri jinsi ilivyo muhimu kwa watu wote kupata haki za msingi za kibinadamu kama vile maji safi na mifumo salama ya usafi wa mazingira. Sisi sote tunastahili kuwa na afya njema!

Mtangazaji 1: Wiki ijayo tarehe [TAJA SIKU] saa [TAJA SAA] tutakuwa tunazungumza kuhusu [TAJA MADA YA WIKI IJAYO]. Hadi wakati huo, kwaheri!